



Julai 2016

Mpendwa Muombaji,

Hivi karibuni, nilipata muda wa matumaini nilipokumbushwa kuwa hazina tuliyonayo ndani ya Yesu inafunuliwa kupitia maisha yaliyovunjika. Hi ni kwa sababu nguvu za kuokoa hutoka kwa Mungu na sio kwetu sisi (2 Wakorintho 4:7). Kwenye mstari huu, Paulo analitia moyo kanisa la Korintho kwa habari njema kuwa matumaini na uponyaji huwezekana kupitia kwenye wokovu ndani ya Yesu na kwenye maisha yetu ya kawaida, anayoyalinganisha na chungu cha kawaida kilichotengenezwa kwa udongo wa mfinyanzi kinachovunjika kwa urahisi tu.

Nilinyenyekezwa kufikiria kuwa Paulo alitambua jinsi alivyokuwa hana thamani ukilinganisha na neno kuu la matumaini ndani ya Yesu (Waefeso 3:7–9). Naamini Mungu anahitaji tutambue tofauti hii ili lisiwepo swali la chanzo cha injili na nguvu zake; Wokovu ni kazi ya Mungu, siyo yetu (1 Wakorintho 2:5; 3:7).

Lakini tunaishije maisha yaliyojaa matumaini ndani ya nguvu takatifu wakati tunapokabiliwa na changamoto na mateso kila siku?

Tembea kwa imani sio kwa kuona. Kitu kilichomuwezesha Mtume Paulo ulikuwa ni uelewa kuwa maisha ya hapa duniani ni ya kitambo tu (2 Wakorintho 4:18). Paulo aliwatia moyo watu wa kanisa la Wakorintho pamoja na sisi kuwa tusiangalie mazingira yetu magumu lakini tuyatazame maisha yajayo tuliyo nayo pamoja na Yesu. Haya yalikuwa maisha ya Paulo. Kama angekuwa na uchaguzi, angetamani kuachana na ulimwengu na kukaa nyumbani na Bwana (Wafilipi 1:21–23). Umewahi kujisikia hivyo? Najua nimewahi wakati wa kujaribiwa lakini nahuishwa kujua kuwa wanawake na wanaume ulimwenguni kote wanaomba na kumwambia Mungu atupe uweza, matumaini na uponyaji katikati ya majaribu na mateso.

Vumilia kwa kuwa kuna thawabu. Kama Paulo alivyoshirikisha habari njema kwa ulimwengu, watu wengi zaidi wakajifunza na kupokea wema na huruma za Mungu. Wengi waliousikia ujumbe waliitikia kwa kuamini, kupokea wokovu na walishukuru (Waefeso 1:6, 12, 14). Leo hii, tunakutana na kitu hicho hicho tunapoishi maisha ya kutegemea neno la Mungu na kuamini kuwa ipo zawadi kubwa kuliko mateso haya ya muda (2 Wakorintho 4:16–17). Na tuendeleo kuonyesha neema kwa wengine kupitia maombi na matendo, kuelezea visa vyetu sisi wenyewe vya kupata matumaini na uponyaji ndani ya Yesu.

Kila siku tunaweza kupata muda wa matumaini. Mungu anatembea kwenye maisha yetu kupitia maombi. Hajawasahau dada zetu wa nchini China na ni lazima tuendeleo kuinua mioyo na sauti zetu kwa Bwana kwa ajili yao na majaribu wanayokutana nayo kila siku. Simama imara kwenye imani yako na amini leo kuwa unacho kila kitu unachohitaji ili kuishi maisha matakatifu tunapoegemea kwenye nguvu takatifu tuliyoepewa kupitia ufahamu wa neno la Mungu na kwa Bwana wetu Yesu (2 Petro 1: 3–4).

Mungu awabariki,
Peggy Banks
Mkurugenzi wa Kimataifa Huduma
Project Hannah